# STANDARD EIGHT YEAR 2016

# END-TERM 2,

**KISWAHILI PAPER**
**1HR-40MINS**

Coordinated by KENPRO,
Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E,
Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 |
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website:www.schoolsnetkenya.com

# KISWAHILI TIME: 1HR-40MINS

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

1. Tumia penseli ya kawaida.
2. Hakikisha umeandika kwa karatasi yako:
   (i) JINA LAKO (iii) JINA LA SHULE YAKO
3. Kwa kila swali onyesha jibu sahihi kwa kuchora mstari kwenye herufi uliyopewa

**Chagua jibu sahihi kati ya yale uliyopewa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

Jamii ____1____ zimeoza kuliko uozo wa ____2____. Unapopeleleza hasa mienendo na matendo maovu ya hirimu, kwa asilimia kubwa wadadisi ____3____ mambo wanakisia ____4____ filamu chafu na za kuchukiza zinazoonyeshwa katika runinga zimechangia kwa ____5____ katika utovu wa ____6____.

Binadamu ni kiumbe ____7____ anayestahili kutenda mambo kwa ____8____. Anafaa ____9____ tofauti baina yake na mnyama ambaye ____10____ akili ya kutambua kibaya au kilicho kizuri. Vitendo vya binadamu ____11____ mipaka akatenda mambo ya hayawani basi huchukuliwa kuwa ____12____ na kuitwa mnyama ____13____ ana umbo ____14____ binadamu kwa hivyo ubinadamu au ____15____ ni vitendo vyema sio uzuri wa mwili.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. zetu | B. letu | C. yetu | D. langu |
| 2. | A. wazoga | B. mshoga | C. mzoga | D. mizoga |
| 3. | A. wanapenda | B. wanaona | C. wanaochunga | D. wanaodadisi |
| 4. | A. kwenye mnamo | B. kuwa huenda | C. kama bora | D. ingalikuwa |
| 5. | A. sehemu kubwa | B. seemu kubwa | C. shehemu kubwa | D. sehemu kumbwa |
| 6. | A. nitamu | B. nithamu | C. nidhamu | D. nidamu |
| 7. | A. kilicho lasmi | B. uliye rasmi | C. aliye rasmi | D. kilicho rasimi |
| 8. | A. kufikiria | B. kufikiri | C. kufikirisha | D. kufikiriana |
| 9. | A. kuthihirisha | B. kudhihirisha | C. kudhihilisha | D. kudhilisha |
| 10. | A. amesheheni | B. asiyesheheni | C. shehena | D. anashehena |
| 11. | A. wanapokidhiri | B. zinapokidhiri | C. vinapokithiri | D. anapokidhiri |
| 12. | A. mkatili | B. katili | C. mkatiri | D. katiri |
| 13. | A. isipokuwa | B. ijapokuwa | C. na | D. ila |
| 14. | lisiloashiria | B. linaloashiria | C. linalokataa | D. lisiloelekea |
| 15. | A. utu | B. uchu | C. urembo | D. unyama |

**Kutoka swali la 16 hadi 30 chagua jibu lililo sahihi**

16. Mahali pwani pa kuteremshia abiria huitwa ______________ au gati.
    A. kilindi  B. bunta
    C. kambi  D. ufuo
17. **Teua umoja wa sentensi hii**
    Nyasi zile ni ndefu sana.
    A. Nyasi ili ni ndefu sana.
    B. Nyasi ile ni mrefu sana.
    C. Unyasi ule ni mrefu sana.
    D. Unyasi ule ni ndefu sana.
18. Kuku aliyepita makamo ya utamba na kuanza kutaga mayai huitwa mtetea. Je, kuku ambaye hawezi kutaga mayai huitwaje?
    A. koo  B. kiweto
    C. kiwete  D. gumba
19. Maana ya "kumpa mtu nyama ya ulimi" ni _____?
    A. kumtolea ulimi wa mnyama
    B. kumwonyesha ulimi kwa bezo
    C. kumwambia mtu maneno matamu
    D. kumchekelea mtu kwa kufanya jambo la ajabu
20. Kinyume cha **ganda** ni ____________?
    A. gandika
    B. gando
    C. gandua
    D. yeyuka
21. Kumwepuka mtu kwa dharau na kumwona kama kinyaa au mchafu ni ______________?
    A. kunyanyapaa
    B. kunyanyasa
    C. kunyonyoa
    D. kunyong'onyea
22. **Chagua kielezi katika sentensi ifuatayo**
    Chakula chako ni kitamu mno kuliko changu.
    A. chako  B. kitamu
    C. kuliko  D. mno
23. **Andika udogo wa sentensi hi**
    Kichwa chake ni kikubwa.
    A. Vichwa vyao ni vikubwa
    B. Jichwa lake ni kubwa
    C. Majichwa yao ni makubwa
    D. Kijichwa chake ni kikubwa
24. Neno **karai** liko katika ngeli gani?
    A. I - ZI  B. LI - YA
    C. U - ZI  D. I - I
25. **Andika kwa maneno.**
    9,000,000,000
    A. Bilioni tisa  B. Milioni tisa
    C. Elfu mia tisa  D. Laki tisa
26. Nilikuwa wa kwanza kuwasili shuleni. Hiyo basi nilifika __________ watu wote.
    A. baada ya  B. mbele ya
    C. kabla ya  D. nyuma ya
27. **Kamilisha methali**
    Siku ya nyani kufa ________________
    A. wengine huforoka
    B. huwa mkali sana
    C. hutembea peke yake
    D. miti yote huteleza
28. Masalkheri ni maamkizi ya wakati gani?
    A. Asubuhi  B. Jioni
    C. Usiku  D. Alfajiri
29. **Tukisema kuwa;-**
    Mwanasada na Mwanaimani ni rupia kwa ya pili tuna maana ______________?
    A. wanafanana sana
    B. wanatofautiana sana
    C. wawnalingana sana
    D. hawapendani
30. Oloo ni fisi. Tamathali iliyotumika ni ________?
    A. tashbihi  B. stiara
    C. naha  D. takriri

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40**

Watu waliokuwa na makunyanzi ya kutisha walikuwa wametuzingira. Mafinyo hayo yalikuwa yamehinikiza ghadhabu na nikaanza kutetemeka te!te!te! Nililemewa na nikatunduwaa nikakuna kichwa, nikawaza na kuwazua kile ambacho ningefanya. Nilimwona kaka yangu akinitazama kwa hasira na moyo ukatutusa na kututa. Katika kijiji chetu siku hiyo, wasichana walikuwa wakipashwa tohara na nilikuwa mmoja wao. Woga ulikita mizizi na nikakata kauli kuchana mbuga. Watu waliniona na kunifukuza kama swara afukuzwaye na chui. Walinishika na wengi walikuwa na hamu ya kunipiga kipopo. Nilikuwa nimeamua kuwa nisingefanyiwa kitendo hicho cha unyama.



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

Niliinuliwa na kubebwa hangahanga na ndugu yangu wa toka nitoke. Kweli ibilisi wa mtu ni mtu. Nilirudishwa kijijini petu ambapo watu walikuwa wakiimba kwa furaha. Kwa bahati nzuri, afisa wa elimu ya vijana na haki za jinsia aliwasili. Alikemea kitendo kile cha ukeketaji na akatishia kuwaita polisi endapo wangeendelea na kitendo kile. Niliponea chupu chupu.

Hata hivyo bado mtego mwingine ulikuwa ukiningoja. Ndoa ya lazima ilikuwa ikiningoja. Nilikata shauri kutoroka ili kuepuka kuolewa. Nilifahamu fika kuwa, mwenzako akinyolewa, tia chako maji. Wenzangu wengi walikuwa wametaabika baada ya kuolewa. Nilitarajiwa kuolewa na mzee mmoja aliyebugia chumvi si haba. Tayari alikuwa na wake watatu. Hata hivyo, hapakuwa na njia ya kutoroka. Basi ikawa lisilo budi hubidi.

Siku yenyewe ilifika. Tulianza kutayarisha sherehe. Watu walikuwa wakichapa kazi kwa bidii sana huku wakiwa wenye furaha. Nilipukutikwa na machozi ya jitimai puku! puku! Niliwalaani wahusika lakini hiyo ilikuwa ni dua ya kuku kwa mwewe.

Harusi ya kitamanduni iliandaliwa barabara mara bwana harusi akakabidhiwa mke wake kwa shangwe na hoihoi. Ghafla bin vuu, chifu aliwasili na askari. Wazazi wangu pamoja na bwana harusi walitiwa mbaroni nami kuachiliwa huru huku nikiambiwa niendelee na masomo yangu. Niliamini kweli mila nyingine ni potuvu.

31. Makunyanzi yanaweza kusababishwa na uzee, vivyo hivyo yanaweza kusababishwa na _____?
    A. ujana B. furaha
    C. hasira D. ujanja
32. Msemaji alishangaa na kukasirika kwa nini?
    A. alikuwa afanyiwe tohara ya lazima
    B. tohara kwake ilikuwa hiari
    C. watu wengi walikuwa karibu naye
    D. nduguye alikuwa ak mwangalia
33. Ni kweli kusema kuwa _________
    A. kakaye alikasirishwa na tohara
    B. wazazi hawakufahimishwa kuhusu tohara hiyo
    C. kakaye aliunga mkono tohara hiyo
    D. wanakijiji wote walipinga tohara ya wasichana
34. Kupigwa kipopo ni ____________?
    A. kupigwa kama popo
    B. kupigwa na watu wengi
    C. kupewa adhabu kali
    D. kufunzwa adabu
35. Tohara ilisitishwa kwa kuwa ___________
    A. wenyeji walikuwa waende safarini
    B. kulikuwa na sherehe za kitaifa
    C. chifu hakuwa amefahamishwa
    D. ni mila potovu zinazowabeza wasichana
36. Nyimbo za watu zinaonyesha _________
    A. kuunga mkono kwao
    B. kughadhabika kwao
    C. hasira zao
    D. upinzani wo
37. Kwa nini msichana alitaka kutoroka?
    A. aliteseka sana baada ya kuolewa
    B. hakutaka kuolewa na mzee yule
    C. alikuwa na hamu ya kuolewa
    D. ndoa ilikuwa imecheleweshwa sana
38. Kama msichana yule angeolewa angekuwa mke wa ngapi?
    A. wa kwanza B. wa pili
    C. wa tatu D. wa nne
39. Neno jingine lenye maana sawa na jitimai ni ____
    A. machozi B. majonzi
    C. siahi D. kamsa
40. Habari hii inaonyesha jamii ambayo _______
    A. inathamini haki za wasichana
    B. haithamini dhuluma za wasichana
    C. haithamini kazi za wasichana
    D. inapenda sana elimu ya wasichana



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

**Soma habari hii kisha ujibu maswali 41 - 50**

Nilizaliwa katika familia ya walalaheri. Wavyele wangu walinifaa katika dhiki na faraja, kwa hali na mali. Sikupata masaibu katu na niliishi maisha ya raha mustarehe. Hata hivyo, raha yangu iligonga mwamba wazazi wangu walipokata kamba katika ajali ya barabarani. Vifo hivyo vya ghafla bin vuu, vilibadilisha maisha yangu. Ukwasi wa wazazi wangu ulitoweka kwa sababu sikujua jinsi walivyopata pesa zao. Hakuna aliyenijali, marafiki wa baba na mama yangu walitoweka kama umande jua linapochomoza.

Kwa nyota ya jaha, babu yangu alinifadhili kwenye nyumba yake. Faraja iliyoje? Babu alikuwa mzee aliyebugia chumvi si haba. Aliishi na nyanya aliyekuwa mzee. Walikuwa walala hoi. Nilishangaa kwa nini wazazi wangu hawakuwasaidia walipokuwa hai. Tulikuwa tukila na kusaza ilhali babu na nyanya walikuwa wakiteseka. Mawazo hayo yalinisumbua sana. Hata hivyo, walishirikiana kama mchi na kinu kunilea japo walipata shida tele. Nilipokosa, waliniadhibu kwani zinguo la mtukutu ni ufito.

Niliamua kusoma kwa bidii sana ili nifaulu na kuwasaidia babu na nyanya. Walinifaa kwa hali na mali. Babu alijotolea kuwauza mbuzi na ng'ombe kunilipia karo nami niliamua pesa hizo haziwezi kupotea bure. Nilikuwa na jukumu la kuwatunza hata ijapokuwa wazazi wangu walishindwa kufanya hivyo. nilifaulu katika kidato cha nne na kuenda chuo kikuu kusomea udaktari. Nilifaulu kuwa daktari na kupata kazi nzuri sana.

Kamwe nisingeweza kupoteza ahadi yangu. Niliwajengea nyumba nzuri. Niliwaajiri wafanyakazi wa kuwasaidia nyumbani na shambani. Niliamini kuwa mili yetu ni kama mimea. Ikitunzwa inanawiri vyema. Wazee hawa walibadilika na kuwa kama vijana. Waliishi maisha ya raha na starehe. Walifurahia juhudi walizofanya kumtunza mjukuu ambaye kwa sasa amefanya uzee wao kuwa wa vicheko na furaha.

41. Tunaweza kusema kuwa familia ya msemaji ilikuwa ____ ________
    A. katika hali ya ukwasi
    B. katika hali duni ya umaskini
    C. jamii ya ombaomba
    D. jamii iliyowajali nyanya na babu
42. Ni nini kilichokatiza furaha ya msemaji?
    A. masaibu
    B. vifo vya wazazi
    C. kukosa masomo
    D. sherehe
43. Wavyele wa msemaji wanaweza kupigiwa mfano wa methali isemayo ____________
    A. Mwenda pole hajikwai
    B. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
    C. Hayawi hayawi huwa
    D. Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi
44. Marafiki wa wazazi wa msemaji walikuwa ____
    A. wanzuri na wanyenyekevu
    B. wengi na waliomfaa katika dhiki
    C. waongo ambao wasingemfaa katika dhiki
    D. waliomfaa sana kwa dhiki
45. Mama aliyebugia chumvi si haba ataitwaje?
    A. ajuzua B. shaibu
    C. buda D. mjuzi
46. Ni nini kilichosumbua mawazo ya msemaji?
    A. vifo vya wazazi wake
    B. maisha ya umaskini ya babu na nyanya yake
    C. masomo yake ambayo yalitumbukia nyongo
    D. marafiki waliojitolea kumsaidia wakati wa dhiki
47. Ni nini maana ya neno <u>**kusaza**</u>?
    A. kuharibu
    B. kushiba
    C. kuchoka
    D. kubakiza
48. Kuadhibiwa kwa msemaji kunaonyesha ____?
    A. upendo B. chuki
    C. heshima D. ukali
49. Ni kweli kusema kuwa wazazi wa msemaji _____?
    A. walitunza wazazi wao
    B. walikuwa na watoto wengi
    C. hawakuwatunza wazazi wao
    D. walikufa baada ya kuugua kwa muda mfupi
50. Ni methali gani inafaa kuambiwa babu na nyanya ya msemaji?
    A. Kipya kinyemi kingawa kidondo
    B. Baada ya dhiki faraja
    C. Kizuri cha jiuza kibaya cha jitembeza
    D. Cha mlevi huliwa na mgema



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27